# MFUKO WA ELIMU

Toleo Maalum

Feb. 2026

## SIKU 100

...za Uongozi wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
ndani ya **Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**








**"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu ya Elimu"**



^^^^^ *Pichani ni Mhe Rais Dr Samia Suluhu Hassan akila kiapo tarehe 03.11.2025 Jijini Dodoma.*

Tarehe 3 Novemba 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliapishwa rasmi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Uongozi wake umeendelea kuonesha dira ya dhati ya kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hususan katika sekta ya elimu ambayo ni nguzo muhimu ya maendeleo ya Taifa.

Tunapoadhimisha siku 100 za uongozi wa Mheshimiwa Rais baada ya uchaguzi mkuu, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kama mojawapo ya taasisi za umma, inayosimamia Mfuko wa Elimu wa Taifa imeendelea kuchukua hatua madhubuti kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji nchini. Hatua hizi zinaenda sambamba na mkakati wa kuandaa kizazi chenye maarifa, ujuzi na uwezo wa kujitegemea.




**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti**
Bw. Masozi Nyirenda

**Mhariri**
Bi. Bestina Magutu

**Wachangiaji**
Bi. Eliafile Solla

**Anuani**
Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),
S.L.P 2516,
Dodoma - Tanzania.

Tovuti: www.tea.or.tz
Barua pepe: info@tea.or.t





**M**iongoni mwa hatua zilizofanyika ndani ya siku 100 ni **kutenga shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya mafunzo ya amali katika shule 19 za sekondari nchini.** Uwekezaji huu unaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuimarisha ufundishaji wa masomo ya amali, ambayo yameendelea kutambuliwa kama mhimili muhimu wa kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi wa vitendo unaokidhi mahitaji ya soko la ajira na ujasiriamali.
Hatua hii ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuimarisha masomo ya amali, sambamba na ahadi alizozitoa ndani ya siku 100 za uongozi wake. Kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, TEA inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo katika shule 19 za sekondari zilizopo katika mikoa 15 kote nchini, ambapo jumla ya wanafunzi 1,810 watanufaika moja kwa moja, wakiwemo wasichana 647 na wavulana 1,163.

Uboreshaji wa miundombinu ya amali unahusisha ujenzi na ukarabati wa majengo pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu inayochanganya nadharia na vitendo, hivyo kuwajengea ujuzi wa kujiajiri, kuajirika au kuanzisha miradi ya uzalishaji mara baada ya kuhitimu.



<<<<<^^^^^ *Pichani ni baadhi ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia mafunzo ya Amali katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe*

Aidha, mpango huu unaendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 inayolenga kujenga jamii yenye ujuzi, bunifu na yenye uwezo wa kushindana katika uchumi wa kikanda na kimataifa.




Moja ya shule zilizonufaika na utekelezaji wa miradi hii ni Shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe, iliyopo katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe, ambayo ilipokea ruzuku ya shilingi 421,089,900 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya fani za upishi, kilimo cha mbogamboga, teknolojia ya ubunifu na ushonaji. Upatikanaji wa vifaa hivi umeongeza hamasa na idadi ya wanafunzi wanaochagua mikondo ya amali, hali inayochochea wasichana kujifunza stadi zitakazowawezesha kujitegemea kiuchumi na kuchangia maendeleo ya jamii zao.


Vilevile, Shule ya Sekondari Nkowe iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ilinufaika kwa kupokea ruzuku ya shilingi 66,650,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya michezo (mpira wa miguu na mpira wa pete) pamoja na ujenzi wa kiwanja cha mpira wa pete. Mradi huu umechangia ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na amali ya michezo, huku kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja kukiwa fursa ya kuibua vipaji na kukuza taaluma ya michezo kuanzia ngazi ya shule.



Shule nyingine zilizopata ufadhili wa TEA kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mafunzo ya amali ni Chief Sarwatt - Mbulu TC, **(Sh.181,020,000),** Shule ya Sekondari ya Kutwa Arusha -Arusha CC, **(Sh. 44,152,000),** Shule ya Sekondari Darajani -Moshi DC **(Sh. 67,359,000),** Shule ya Sekondari Usangi Mwanga DC **(Sh. 44,152,000.00),** Shule ya Sekondari Shule ya Sekondari Dar es Salaam - Dar es Salaam CC **(Sh. 44,152,000),** Shule ya Sekondari Matola - Njombe TC **(Sh. 66,650,000).**

Shule nyingine zilizofadhiliwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mafunzo ya amali ni Shule ya Sekondari Uwemba, Njombe TC **(Sh. 280,822,400),** Shule ya Sekondari Mbeya, Mbeya CC **(Sh. 66,650,000),** Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga, Mbeya CC **(Sh. 276,258,511),** Shule ya Sekondari Msangano, Momba DC **(Sh. 265,979,900),** Shule ya Sekondari Ukombozi, Uyui DC, **(Sh. 66,650,000),** Shule ya Sekondari Kigoma- Kigoma MC **(Sh. 66,650,000).**

Nyingne ni Shule ya Sekondari ya Wavulana Bwiru-Mwanza CC **(Sh. 229,241,511),** Shule ya Sekondari ya Pamba - Mwanza CC **(Sh. 199,812,000),** Shule ya Sekondari ya Wasichana Iringa - Iringa MC **(Sh. 199,812,000),** Shule ya Sekondari Morogoro - Morogoro MC **(Sh. 66,650,000),** Shule ya Sekondari Mafiga -Morogoro MC **(Sh.280,822,400).**




*^^^^^ Pichani ni baadhi ya vifaa vya muziki kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia mafunzo ya Amali katika Shule ya Sekondari ya Darajani, Moshi .....*








Mbali na miradi ya ujenzi wa miundombinu ya mafunzo ya amali, Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na TEA unatekeleza miradi mingine 633 ya ujenzi wa maabara za sayansi, vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, mabweni na matundu ya vyoo yote ikiwa na thamani ya Sh. Bilioni 11.73 katika Mwaka wa Fedha wa 2025/ 2026.

Miradi hii ni muhimu kwa vile Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 imebainisha wazi kuwa ,rasilimali watu yenye ujuzi na maarifa ndiyo msingi wa kufikia maendeleo endelevu. Jamii iliyoelimika, yenye uwezo wa kubuni na kutatua changamoto kwa vitendo, imewekwa kuwa miongoni mwa vipaumbele vya sekta ya elimu. Ndani ya muktadha huu, masomo ya amali yanachukua nafasi muhimu katika kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira, kukuza ujasiriamali na kuimarisha uchumi wa Taifa.

Kutokana na umuhimu huo, TEA itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya umma na binafsi katika kutafuta rasilimali za fedha na vifaa, ili kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mafunzo ya amali nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa vipaumbele vyote vya sekta ya elimu vinavyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 vinafikiwa kwa usawa katika maeneo yote ya nchi.



^^^^^ *Muonekano wa jengo la madarasa yaliyojengwa na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa katika Shule ya Msingi Kazaroho iliyopo Wilayani Kaliua mkoani Tabora*




^^^^^ *Muonekano wa jengo la maabara mbili za masomo ya sayansi (Biolojia na Kemia) katika Shule ya Sekondari Itumba, Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Mkoa wa Songwe, limekamilishwa kwa ufadhili wa UNICEF kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).*





Mamlaka ya Elimu Tanzania inaendelea kuzingatia azma ya Serikali ya kuhakikisha elimu inayotolewa katika ngazi zote ni bora, jumuishi na inayomuwezesha mhitimu kukabiliana na mazingira halisi ya maisha. Azma hii inaendana na Lengo la Nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu Duniani (SDG 4), linalosisitiza elimu bora, yenye usawa na fursa kwa wote. Hakika, uwekezaji katika elimu ya amali ni uwekezaji wa moja kwa moja katika maendeleo ya watu na Taifa kwa ujumla.





^^^^^ *Pichani ni muonekano wa miundombinu mbalimbali ya elimu iliyojengwa na TEA kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia*

^^^^^ *Ifuatayo ni baadhi ya miundombinu ya kujifunzia na kufundishia iliyoboreshwa na UNICEF kwa kushirikiana na TEA*





***Picha kubwa** ni muonekano wa choo kwa ajili ya wanafunzi katika Shule ya Msingi Kagondo mkoani Kigoma. Picha ndogo ni muonekano wa choo kilichokuwa kikitumika awali kabla ya kujengwa kwa choo kipya ambacho **kimefadhiliwa na fedha kutoka Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ushirikiano na UNICEF.***



*Muonekano wa Bweni la Wasichana katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kakonko - Kigoma*



***Pichani** ni matundu ya vyoo katika Shule ya Msingi Tangazo mkoani Mtwara*






***Pichani** ni jengo la bweni Shule ya Sekondari Malocho, mkoani Mtwara*









***Pichani** ni mwalimu akiendelea kufundisha katika Shule ya Msingi Umoja mkoani Lindi. Ujenzi wa vyumba vya madarasa hayo umefadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa*

## Tufuatilie Kupitia Mitandao Yetu Ili Kupata Taarifa Zaidi


officialteatz

officialtea_tz

www.tea.or.tz

info@tea.or.tz